**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

# MIAKA 2 YA UONGOZI WA RAIS NA MAFANIKIO KWENYE ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

2021 - 2023



**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

VETA



# Miaka Miwili ya Uongozi wa Rais Samia: Wananchi waongezewa fursa za kujipatia ujuzi

- **Vyuo 33 vya VETA vya Wilaya na Mikoa vyajengwa na kuwekewa samani**
- **Zaidi ya vijana 155,000 wapatiwa ujuzi kupitia ufadhili wa Serikali na tozo ya ujuzi**

Miongoni mwa mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuwawezesha wananchi kujipatia ujuzi. Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake, Mhe. Rais ameendelea kutoa kipaumbele kikubwa kwenye elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kuhakikisha watanzania wanajipatia ujuzi utakaowawezesha kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuwezesha vijana kujiajiri.

Dhamira hii ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuonekana kwa vitendo kupitia jitihada na mikakati mbalimbali iliyowekwa ya kuhakikisha fursa za watanzania kujipatia ujuzi zinaongezeka na kuwafikia kwenye maeneo yao wanayoishi.

Akizungumza wakati akizindua Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera, tarehe 13 Oktoba, 2022, Mhe. Rais alisisitiza juu ya nia yake ya kuhakikisha vijana wanapata ujuzi ili kutengeneza nguvu kazi itakayoweza kujiajiri na kuajiriwa.

"Tunazungumzia tatizo la kutokuwa na ajira, tunasomesha watoto lakini hawana ajira… Kazi yetu ni kuhakikisha tunawajengea uwezo vijana kwa kuwapatia ujuzi ili waweze kujiajiri na kuajiriwa," alisema.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 umeainisha uendelezaji ujuzi kupitia mafunzo ya ufundi stadi kama hatua muhimu katika kuhakikisha uzalishaji wa rasilimaliwatu nchini na kuwezesha vijana kujiajiri.





Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), CPA. Anthony Kasore anaeleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa katika kuhakikisha ujuzi unawafikia watanzania pale walipo kwa kuwasogezea vyuo vya ufundi stadi kupitia ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi kila Wilaya nchini.

"Tumeshuhudia msisitizo aliouweka Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kuhakikisha vijana wanapata ujuzi ambao anaamini kabisa kuwa utaiwezesha nchi kuwa na rasilimaliwatu yenye kuongeza tija katika uzalishaji, kutatua changamoto ya ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa nchi,"amesema

CPA. Kasore anataja ujenzi wa vyuo vya Ufundi stadi vya Wilaya na Mikoa, utoaji wa ujuzi bila gharama kwa makundi mbalimbali katika jamii, uimarishaji wa ubora wa utoaji mafunzo ya ufundi stadi, ununuzi wa mitambo na zana za kisasa za kufundishia pamoja na uendelezaji ubunifu miongoni mwa mambo makubwa ya kujivunia kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwenye eneo la Ufundi Stadi.

# Ujenzi wa vyuo 33 vya Ufundi Stadi vya Wilaya na Mikoa

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imewezesha kukamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya ufundi stadi vya Wilaya za Ruangwa,Nyasa,Kasulu,Kongwa,Chunya,Kilindi, Korogwe, Ukerewe, Igunga, Pangani, Kishapu, Rufiji, Uyui, Kwimba, Bahi, Mafia, Longido, Mkinga, Uvinza, Ikungi, Iringa Vijijini, Lushoto, Mbarali, Monduli, Buhigwe, Ulanga, Masasi, Butiama na Chemba pamoja na vyuo vya Mikoa ya Njombe, Rukwa, Simiyu na Geita. Jumla ya Shilingi Bilioni 94.5 zilitumika katika kuwezesha ukamilishaji wa ujenzi wa vyuo hivyo. Vyuo 25 vya ufundi stadi vya wilaya vimejengwa na VETA kwa kutumia nguvu kazi ya ndani (Force Account).

Vyuo hivyo 33 vinatarajiwa kuleta ongezeko la wanafunzi 46,675 katika udahili kwenye vyuo vya VETA.



MUONEKANO WA CHUO CHA VETA UKEREWE

# MUONEKANO WA VYUO VYA VETA



VETA UKEREWE



VETA ULANGA



VETA BUTIAMA



VETA KILINDI

UJENZI KWA
KUTUMIA FORCE
ACCOUNT



VETA KWIMBA

# Uimarishaji wa Ushirikiano wa Kidiplomasia: Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera chajengwa kwa hisani ya Serikali ya Watu wa China

Uimarishaji wa ushirkiano wa kidiplomasia pia umewezesha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera kupitia ufadhili wa Serikali ya Watu wa China kwa gharama za shilingi bilioni 22.

Ujenzi wa chuo hicho umekamilika na mafunzo yameanza kutolewa. Chuo kina uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 800 wa kozi za muda mrefu na wanafunzi 1,000 wa kozi za muda mfupi. Pia kinaweza kutoa Huduma ya malazi kwa wanafunzi 320 ikiwa wa kike 104 na wa kiume 216.



## Ujenzi wa vyuo 64 vya Ufundi Stadi vya Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe

Serikali ya Awamu ya Sita ilitenga shilingi bilioni 100 katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo 64 vya ufundi stadi vya Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe ili kutimiza azma yake ya kuhakikisha Wilaya zote na Mikoa yote inakuwa na vyuo hivyo. Kukamilika kwa ujenzi wa vyuo hivyo kunatazamiwa kuongeza fursa zaidi za utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.



Ujenzi wa vyuo hivyo unatarajiwa kuchangia ongezeko la wanafunzi 89,700 katika udahili wa vyuo vya VETA.

## Utekelezaji wa programu za kuwapatia wananchi ujuzi kwa gharama za Serikali

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuwawezesha wananchi wa makundi mbalimbali kujipatia ujuzi. Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, jumla ya vijana 155,000 wamenufaika na mafunzo kwa ufadhili wa Serikali, tozo ya ujuzi na kwa kupitia ushirikiano na wadau.



Vijana 140,124 wamepata mafunzo kwenye vyuo vya VETA kupitia tozo ya kuendeleza ujuzi.

Kupitia Mpango wa Uanagenzi ulioratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) vijana 10,456 walifadhiliwa kupata mafunzo katika vyuo vya VETA huku vijana wengine 420 wakinufaika na mafunzo ya teknolojia ya kutengeneza vihenge vya chuma (metal silos) kwa ajili ya kuhifadhia mazao ili kutatua changamoto ya usalama wa chakula hususani udhibiti wa Sumukuvu.

Mwezi Desemba,2022, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) na VETA,ilitangaza ufadhili kwa wanafunzi 4,000 kupitia mradi wa kikanda wa Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo ya Afrika (E4D) ambao wanaendelea na mafunzo kwenye vyuo mbalimbali vya VETA.



# Uimarishaji wa ubora wa mafunzo ya ufundi stadi

Sambamba na upanuzi wa fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi, suala la ubora wa mafunzo yanayotolewa pia limeendelea kutiliwa mkazo. Katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita, jitihada mbalimbali za kuimarisha ubora wa mafunzo zimefanyika kupitia uhuishaji wa mitaala ya kufundishia pamoja na ununuzi wa mitambo, zana na vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia. Jumla ya mitaala 48 imehuishwa ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira na mwenendo wa nchi kiuchumi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, amekuwa mstari wa mbele kuhimiza watendaji wa Wizara na taasisi zake kuweka na kutekeleza mikakati mbalimbali yenye kutafsiri kwa vitendo maono ya nchi kuhusu elimu ujuzi. Akiwa katika kikao cha kutathmini utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyuo 25 vya ufundi stadi vya wilaya na kujadili kuhusu ujenzi wa vyuo 64 vya ufundi stadi vya wilaya na kimoja cha mkoa wa Songwe kwenye ukumbi wa Chuo cha VETA Dodoma, tarehe 17 Novemba 2022, Prof. Mkenda aliwasa watendaji kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo ili utekelezaji wa maono ya elimu ujuzi uonekane wazi.

"Nchi yote sasa inazungumza kuhusu elimu ujuzi ambapo kiuhalisia ni ufundi stadi," alisema. Sambamba na hilo, Prof. Mkenda aligusia mapendekezo ya Sera mpya ya Elimu na kusema kuwa suala la ufundi stadi limepewa kipaumbele kikubwa.



## Uendelezaji Ubunifu




Serikali ya Awamu ya Sita inatambua umuhimu wa vipaji na ubunifu kwa vijana wa kitanzania na mchango wake katika maendeleo ya nchi.

Miongoni mwa wabunifu hao ni walimu na wanafunzi wa vyuo vya VETA nchini ambao wamekuwa wakibuni vifaa, zana na teknolojia mbalimbali kutokana na kutumia muda mwingi kwenye karakana za mafunzo. Ubunifu wao umelenga kutatua changamoto mbalimbali katika jamii na kurahisisha shughuli za kiuchumi.Jumla ya wabunifu 25 wa ufundi stadi waliibuliwa na kuendelezwa na Serikali kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) katika kipindi cha mwaka 2021 na mwaka 2022. Miongoni mwa bunifu za walimu na wanafunzi wa VETA zilizowezeshwa ma kufikia hatua ya matumizi ni pamoja na Kifaa cha Umwagiliaji mashamba; Kifaa cha kupuliza dawa za kuua wadudu kwenye mimea kinachotumia umeme wa jua; mashine ya kukausha vyakula na mbogamboga; mashine ya kuzidua ubuyu; kifaa cha kufukuza ndege waharibifu mashambani; mashine ya kutengeneza chakula cha samaki na mashine ya kufungasha viungo.



CPA. Kasore anaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kipaumbele kikubwa kwenye elimu na mafunzo ya ufundi stadi na kusema kuwa VETA itaendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa ufanisi na kuhakikisha watanzania wengi zaidi wanajipatia ujuzi na kushiriki vyema kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi.







# UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA

VETA